DAMU YA YESU KRISTO IMELETA ONDOLEO LA DHAMBI

Mwandaaji: KAMANA PAUL

Mawasiliano 0744262394 WhatsApp

YouTube: Kamana Gospel Mission

Facebook:Ev Y N Kamana Ministry

Waebrania 9:22 ***Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo***

Mambo ya Walawi 16, Kutoka 28, Kutoka 30

Dhambi nini?

Dhambi ina maanisha kukosea alama, alama ni kiwango cha MUNGU ama mpango wake hivyo ukienda kinyume na mapenzi ya MUNGU hiyo ndiyo Dhambi.

Mungu ana mipango tofauti kwa watu tofauti hivyo hata alama zinatofautiana yapo mambo ambayo tunachangia wote kwa ujumla kama binadamu na vipo vitu vilivyo juu ya kanisa na kisha huja mtu binafsi.

Dhambi ya asili iliyo tendwa na Adam una Eva ilileta uharibifu wa mahusiano kati ya Mungu na mwanadamu, Mungu akiwa Baba, Bwana, na Mfalme, alizingatia maumbile ya mwanadamu na akahakikisha kwamba anatoa njia ya sisi kubaki katika ushirika naye.

Hapo ndipo linakuja suala la damu kama ondoleo la dhambi, Dhambi isingeweza kusamehewa bila kumwaga damu. "Kwa kweli, chini ya sheria karibu kila kitu hutakaswa kwa damu, na bila ya kumwaga damu hakuna msamaha wa dhambi. ” (Waebrania 9:22)

maswali huja kwanini jibu kuu na sahihi ni kuwa mshahara wa dhambi ni mauti (Warumi 6:23) na mauti ilipo huondoa uhai lakini uhai wa kitu upo ndani ya damu

Mwanzo 9: 4 ***Bali nyama pamoja na uhai, yaani, damu yake, msile.***

Hivyo ilitakiwa damu isiyo na hatia iweze kumwagika kwa ajili ya wengi nayo si nyingine bali damu ya Yesu Kristo kabla ya damu hiyo kuja kulikuwa na shida kweli kwa wayahudi mambo yalikuwa hivi

VITU MUHIMU VILIVYO ZINGATIWA ILI KULETA UPATANISHO NA ONDOLEO LA DHAMBI

YOM KIPPUR, (Siku ya Upatanisho)

Ulikuwa ni mwaka wa Klyahudi wenye mfungo mgumu zaidi wa kidini ulikuwa na siku kumi za toba zinazoanza na **Rosh Hashanah** (Mwaka Mpya wa Kiyahudi). Siku hii,Wayahudi wanamuomba Mungu msamaha kwa dhambi zao ili kupata hatima yao. Inajulikana pia kama Sabato ya Sabato (Sabath of Sabbaths) ilichukuliwa kuwa siku takatifu zaidi ya mwaka wa Kiyahudi. Mada zake kuu ni upatanisho na toba hapo ndipo ilikuwa lazima kuzikumbuka sabato zote

Kutoka 20: 8-11

Upatanisho ulio fanyika ulikuwa unashughulikia maeneo matatu kuhani mkuu, patakatifu, na watu wote.

Kwa mara ya kwanza upatanisho kwenye Biblia tunarejerea Kutoka 30 mistari tisa ya mwanzo inafafanua namna ambavyo Madhabu ya Uvumba ianavyo paswa kuwa hapo linatolewa onyo kali juu ya namna uvumba unavyotolewa

Kutoka 30: 9-10 ***Hamtafukiza juu yake uvumba mgeni, wala sadaka ya kuteketezwa, wala sadaka ya unga, wala hamtamimina juu yake sadaka ya kinywaji.Naye Haruni atafanya upatanisho juu ya pembe zake mara moja kila mwaka; kwa damu ya ile sadaka ya dhambi ya kufanya upatanisho, mara moja kila mwaka ataifanyia upatanisho, katika vizazi vyenu vyote; ni takatifu sana kwa Bwana***

Madhabahu ya Shaba

ilitengenezwa kwa mti wa MSHITA (shittim) na kufunikwa na shaba. Katika kila pembe zake nne,yalikuwa makadirio, inayoitwa "pembe" **(KERANOT).** Miti ya

Mshita (Shittim au Acacia) ilisifika kwa kuzuia maji na mchwa hivyo pia ilitumika kutengeneza hema lote la kukutania .

Baadhi ya vitu vilivyo tengenezwa na mti wa mshita

1. Sanduku la Agano na miti yake

2. Madhabahu ya shaba na miti yake

3. meza ya mkate wa waonyesho na miti yake

4. Madhabahu ya Uvumba na miti yake

5. Nguzo zote za kutundikia mapazia

6. Nguzo za egemeo / fremu za kusimamia

7. Mlaba ya jedwali

Haya yote ilikuwa ni kivuli kuwa YESU KRISTO atakapo kuja atapelekwa kwenye madhabahu takatifu iliyo undwa na mti wa Mshita yaani msalaba wa kalvari na mambo saba yataegemea kujengwa kwa kutumia mti huo ili kukamilisha hema ya kukutania yaani KANISA

MAMBO AMBAYO KUHANI MKUU ALIFANYA ILI KUKAMILISHA UPATANISHO

(1) Haruni alipaswa kuvua mavazi yake ya kawaida ya kikuhani, kunawa, na kisha avae Mavazi maalumu yaliyotengenezwa kwa kitani ambayo yaliagizwa Kuvaliwa wakati wa kutoa dhabihu katika mahali patakatifu Pa Patakatifu.

Mathayo 27:28-29 ***Wakamvua nguo, wakamvika vazi jekundu. Wakasokota taji ya miiba, wakaiweka juu ya kichwa chake, na mwanzi katika mkono wake wa kuume; wakapiga magoti mbele yake, wakamdhihaki, wakisema, Salamu, Mfalme wa Wayahudi!***

Yesu Kristo alivishwa vazi hilo ilikuonesha kuwa yeye ni kuhani Mkuu anaye tarajia kwenda patakatifu pa patakatifu

(2) Haruni alichukua wanyama wa dhabihu aina mbili muhimu: ng'ombe kwa sadaka yake ya dhambi na mbuzi dume wawili kwa sadaka ya dhambi ya watu wote; kondoo waume wawili, moja ya Haruni na ya pili kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa kwa watu wote

Hapa yatupasa kuelewa Haruni alikuwa si kuhani anaye jitosheleza kuondoa dhambi za ulimwengu wote hivyo alihitaji kuhani mkuu mfano wa Melzedeki atakae ondoa dhambi zote kwa wakati mmoja huyu si yeyote isipokuwa YESU KRISTO.

(3) Haruni alimchinja ng'ombe kwa sadaka yake ya dhambi

Kabla ya mambo mengine ilibidi ajitakase yeye kwanza ndivyo ilivyo mpasa siku zote hapo tunajua pasipo YESU hakuna Kuhani mwingine ambaye angetusaidia wanadamu

(4) Kabla ya kuingia Patakatifu pa Patakatifu na damu ya ng'ombe, Haruni ilibidi aunde "Wingu" la uvumba katika Patakatifu pa Patakatifu, linalofunika kiti cha rehema, ili "kufunika utukufu wa Mungu hivyo hapo ndipo aweze kuingia

Lawi 16:12-13 ***Kisha atatwaa chetezo kilichojaa makaa ya moto yatokayo katika madhabahu iliyo mbele za Bwana, na konzi mbili za uvumba mzuri uliopondwa sana, mikononi mwake, naye atauleta ndani ya pazia. Kisha atatia ule uvumba juu ya moto mbele za Bwana, ili moshi wa ule uvumba ukisitiri kiti cha rehema kilicho juu ya ushuhuda, asije akafa.***

Haruni angekufa papa kwa papo kama angeingia uweponi mwa Mungu bila wingu bandia la uvumba hii ipo kama vile kwa mtu anae enda kulina asali inabidi atengeneze moshi kufuza nyuki ili aweze kuchukua asali je nani angesimama katika uwepo wa BWANA

(5) Kisha Haruni akachukua damu ya yule ngombe-dume na kuinyunyiza juu ya kiti cha rehema mara saba

Haruni ilibidi anyunyize mara saba damu ili kuonesha ukamilifu wa Mungu

(6) Kisha kura zilipigwa kwa mbuzi wawili kuamua ni nani atachinjwa na yupi angeachiliwa huru

Yesu alipigiwa kura je nan I aachiliwe kati yake na Baraba **Mathayo 27:16-17** ***Basi palikuwa na mfungwa mashuhuri siku zile, aitwaye Baraba. Basi walipokutanika, Pilato akawaambia, Mnataka niwafungulie yupi? Yule Baraba, au Yesu aitwaye Kristo***? Basi kura zilimwangukia mbuzi mwororo ambaye ni KRISTO na Baraba aliachiliwa huru kwa kuwa kristo alikuwa yupo kwa ajili ya Baraba asamehewe

(7) Mbuzi wa sadaka ya dhambi ya watu, alitolewa kafara, na damu yake ilikuwa inapelekwa ndani ya Patakatifu pa Patakatifu na kutumika kwneye kiti cha rehema, kama damu ya ng'ombe ilivyokuwa.

Yesu Kristo baada ya kusulubishwa damu yake ilipelekwa patakatifu pa patalatifu mbinguni na ilifanyika huko ondoleo la dhambi kwa watu

(8) Utakaso ulifanywa kwa mahali patakatifu kwa kuonekana kwa kunyunyiza damu ya wote wawili ng'ombe na mbuzi. Upatanisho wa mahali patakatifu unafanywa peke yake, bila mtu yeyote aliyepo kusaidia au kutazama

Yesu Kristo alipo fufuka hakuna mwandamu aliye saidia hapa tunakumbuka juu ya habari za Mariamu Magdalena alipo mwona Yes una kutaka kumgusa alimkataza maana alikuwa bado hajaenda patakatifu pa patakatifu pa mbinguni

Yohana 20:16-17 ***Yesu akamwambia, Mariamu. Yeye akageuka, akamwambia kwa Kiebrania, Raboni! (Yaani, Mwalimu wangu). Yesu akamwambia. Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini***

enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu.

(9) Halafu, nje ya hema, Haruni alipaswa kufanya upatanisho kwa madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, akiitumia , damu ya ng'ombe na mbuzi

Hii inaonesha sio ndani yah ema tu panapo takaswa ila hata hema ya kukutania ambapo watu wote ikiwemo wasio wana wa Israeli walipaswa kukutana palitakaswa ndio maana upatanisho si kwa taifa la Israeli pekee bali kwa watu wote .

(10) **Sasa, mbuzi wa pili, yule aliyehifadhiwa hai, alikuwa na dhambi za taifa kwa kuwekewa mikono na kuhani mkuu juu ya kichwa chake huyu aliachiliwa huru na kufukuzwa atoke kambini huyu mbuzi alipelekwa kwa Azazel.**

Hii ina maanisha ukisha mtwisha dhambi na fadhaa zako Yesu Kristo hazirudi tena milele vipi kuhusu Azazeli huyu alikuwa ni jinni moja kati ya Malaika walio shushwa yeye alikuwa akiona mbuzi aliye twishwa dhambi alikuwa akimwinda

na kumla hapa Wanawaisraeli walikuwa wna baki salama kwanza wasinge weza kuliwa kamwa na Azazeli tena maana kasha mla mbuzi wa dhambi, YESU KRISTO naye baada ya kutwisha dhambi zote za ulimwengu aliingia chini kuzimu kukutana na Azazeli kwa mfano wa shetani mkubwa na kunyanganya mamlaka na funguo ya uzima hapo ndipo kila mwanadamu aliye tua mizigo yake ya dhambi kwa YESU KRISTO haiwezekani tena kuteswa na shetani never na dhambi zilizo ondoka hazirudi tena milele .

(11) Kisha Haruni huingia ndani ya hema ya kukutania, anavua mavazi yake ya kitani, anawa, na kuvaa mavazi yake mavazi ya kawaida ya kikuhani

Baada ya Yesu Kristo kumaliza kazi ya msalaba alirudi tena kwenye nafasi yake kama kuhani mkuu ameketi mkono wa kuume wa MUNGU Baba akifanya tena kazi ya ukuhani ambayo ilikuwa ni maombezi hivyo mpaka sasa hutuombea

Luka 16:19 ***Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.***

(12) Sadaka za kuteketezwa za kondoo waume, moja ya Haruni na jamaa yake na nyingine ya watu sasa inayotolewa

Hii ilikuwa ni sadaka ya kawaida hivyo baada ya upoatanisho sadaka bado inatolewa ndio maana damu ya Yesu Kristo ni hai milele

(13) Dhabihu za mwanzo za ng'ombe na mbuzi zilikamilishwa. Mafuta ya sadaka ya dhambi ilichomwa juu ya madhabahu na mabaki ya ng'ombe na mbuzi walitolewa nje ya kambi, ambapo walichomwa moto .

25 Na mafuta ya sadaka ya dhambi atayateketeza juu ya madhabahu.

.

27 Na yule ng'ombe wa sadaka ya dhambi, na yule mbuzi wa sadaka ya dhambi, ambao damu yao ililetwa ndani ifanye ukumbusho katika patakatifu, watachukuliwa nje ya marago; nao watachoma moto ngozi zao, na nyama yao, na mavi yao.

Mabaki ya dhabihu yalipaswa ya chomwe ndivyo ilivyo dhambi za siri zilizo baki ndani ya mwamini zinapaswa kushghulikiwa kisha mafuta nayo yalichomwa juu

ya mdhabahu hii inaonesha kuwa baada ya kukombolewa tuna hitaji Roho Mtakatifu ndani yetu ili tuweze kudumu katika wokovu .

(14) Wale ambao walikuwa wametiwa unajisi kwa kuwashughulikia wanyama ambao juu yao dhambi za Haruni au watu waliwekewa walikuwa waoga kisha warudi kambini

Lawi 16:26 ***Na mtu yule amwachaye mbuzi wa Azazeli aende zake, ataosha nguo zake, na kuosha mwili wake kwa maji, na baadaye ataingia katika marago***

Wale watu walio husika kumsulubu Yesu Kristo nao pia walisamehewa dhambi zao na kurudi kuhesabiwa wenye haki.

(15) JUKUMU LA WATU KATIKA SIKU YA UPATANISHO (WALAWI 16: 29-34)

1. Kufunga walipaswa kujikana wenyewe (wenyeji na wageni)

2. kujiepushe na kazi

Watu hawakupaswa kuwa wavivu katika Siku ya Upatanisho, ingawa wao (na wale wanaoishi ndani kati yao) walipaswa kushika pumziko la Sabato. Waliamriwa kukumbuka amri hii kama amri ya kudumu kwa "kunyenyekea roho zao.Kuhani mkuu alifanya upatanisho kwa Patakatifu pa Patakatifu, kwa hema ya kukutania (maskani) na mkutano au watu wa Israeli.

Hivyo hakuna wokovu ama ondoleo la dhambi isipokuwa kwa YESU KRISTO pekee

Amina